# Kanuni za Ufundishaji

MWONGOZO 5

## Maendeleo ya Mwalimu Kitaaluma Mafunzo ya Mwalimu

### UTANGULIZI

Mara tu mwongozo wa mwalimu na vitabu vya mwanafunzi vinapotungwa, hatua inayofuata ni kuwaandaa walimu kutumia nyenzo hizi mpya katika madarasa yao. Mafunzo ya kazini na msaada endelevu kwa walimu ni njia bora ya kulifanikisha hili. Mwongozo utajikita katika mafunzo ya walimu ambapo walimu wanakusanyika kwa pamoja ili kujifunza mbinu mpya ya ufundishaji. Mwongozo wa 6 unazungumza kuhusu msaada ambao walimu wanapaswa kupata baada ya mafunzo.

Programu za mafunzo ya walimu zinapaswa kutambua kwamba watu wazima wanahamasishwa na kujifunza kwa namna tofauti na ile ya watoto. Watu wazima wanajiongoza zaidi na wanataka kujifunza mambo ambayo yanaendana na mahitaji yao.[1] Mafunzo yanapaswa kuzingatia vitu ambavyo walimu tayari wanavijua i na vipi wanahitaji kujifunza ili kutumia maarifa hayo mapya. Pia zingatia kwamba walimun tayari wana mzigo wa mambo katika akili zao na hivyo ni kuzingatia idadi ya mambo ambayo akili zao zinaweza kubeba kwa wakati mmoja. Dhana hii ina athari juu ya kiasi cha maudhui na umuhimu wa walimu kuondoka katika mafunzo wakiwa na utambuzi, na pengine hata kutenda kiotomatiki, katika ufundishaji mpya.[2]

Katika mwaka 2017–2018 RTI ilifanya utafiti wa kitaifa kuhusu programu za RTI za mafunzo ya walimu ili kuelewa Zaidi jinsi gani mafunzo ya kazini kwa walimu yamekuwa yakitekelezwa na namna gani yanaweza kuboreshwa.[3] Mwongozo huu unatumia matokeo ya utafiti huokatika kutekeleza namna bora za mafunzo na muundo wa mafunzo yenyewe.

**KANUNI ZA UJIFUNZAJI WA WATU WAZIMA**

1. Zingatia vitu ambavyoo walimu tayari wanavijua
2. Toa fursa ya kuchangia katika maudhui
3. Maudhui yanapaswa kuwa na uhalisia wa hali ya juu
4. IZingatia mbinu z kujifunza kwa vitendo
5. Maudhui yaweze kutumika kwa haraka

Malcolm S. Knowles, *Andragogy in Action: Applying Modern Principles of Adult Learning* (San Francisco: Jossey-Bass, 1984)

### MAUDHUI YA MAFUNZO

**Moja wapo ya maswali ya kwanza ya kuzingatia wakati wa kuandaa mafunzo ni maudhui gani yanapaswa kufundishwa. Kuchagua maudhui muafaka na kuyaandaa kwa namna inayoeleweka, yaendane na kanuni za ujifunzaji za watu wazima, ni muhimu katika kufikia mafanikio ya mafunzo. Maudhui yanapaswa kujikita katika kitu ambacho walimu wanahitaji kujua ili kuwawezesha kutekeleza mbinu mpya za ufundishaji, ikijumuisha vitu maalum ambavyo walimu watahitaji kufundisha watakaporudi madarasani. Utaratibu huu utahakikisha walimu wanajiamini katia kutumia njia hizo mpya darasani.**

#### Uhalisia

Maudhui ya kila mafunzo yanapaswa kuhakikisha uhalisia wa moja kwa moja kwa walimu. Jikite katika maudhui ambayo mwalimu anahitaji kujua ili aweze kufundisha mbinu mpya za ufundishaji, ikijumuisha mada ambazo zitafundishwa katika muhula unaofuata, na wala si kwa mwaka mzima unaofuata, kama hii inawezekana. Mafunzo yajikite kwenye miongozo ya walimu, vitabu vya kiada vya wanafunzi, na shughuli ambazo walimu hao watakuwa wanafanya katika madarasa yao.

#### Kidogo ni kingi

Inashawishi kujumuisha kila kitu tunachotaka walimu kujua katika mafunzo ya mara moja. Lakini, ili kuepuka kuyafanya mafunzo kuwa mzigo mkubwa na kudumisha uhalisia, punguza mjadala wa nadharia. Usijaribu kuweka kila aina ya kipengele cha ufundishaji katika mafunzo ya mara moja. Maudhui yanapaswa kuvunjwa vunjwa kuwa sehemu ndogo ndogo zinazoweza kueleweka kwa uarahisi. Jikite katika shughuli mpya kwa wakati mmoja unganisha muda wa kufanyia mazoezi binafsi kabla ya kujaribu kupitia somo zima la shughuli kwa mara moja.

**KUCHAGUA MAUDHUI SAHIHI NA KUYAANDAA KATIKA NJIA INAYOTEKELEZEKA NI MUHIMU KATIKA KUYAFANYA MAFUNZO KUWA YA MAFANIKIO**

### Fupisha zaidi mafunzo ya mara kwa mara

Mafunzo ya muda mrefu (siku 7–10 au zaidi) yanasababisha walimu kukumbuka sehemu ndogo tu ya kilichofundishwa hapo kabla. **Fupisha, mafunzo ya siku 3–5 mara kwa mara**. Kwa mfano, zingatia kuwa na mafunzo marefu zaidi kidogo (siku 5) ili kuanza mwaka wa masomo na mafunzo mafupi zaidi (siku 3) kipindi cha mapumziko ili kujikumbusha na kuongeza ujuzi mpya. Kufanya hivi kunaipa programu nafasi ya kurekebisha mafunzo ili kuendana na mahitaji ya walimu. Inasaidia kuhakikisha kwamba mafunzo yanalingana na kile ambacho walimu wanakijua tayari, kwamba wana kauli kuhusu maudhui na hujumuisha maudhui wanayohitaji kuyatumia mara moja, katika kuendana na kanuni za ujifunzaji za watu wazima.

## MWONGOZO WA MAFUNZO

**Unapofanya mafunzo ya walimu makumi kwa pamoja na maelfu ya walimu, ni rahisi kwa ujumbe muhimu kupotea. Mwongozo mzuri wa mafunzo unaweza kusaidia kuwa na ujumbe usiobadilika kila hatua ya mafunzo. Hizi hapa ni baadhi ya sifa za mwongozo wa walimu wenye ubora**

### Mfupi na unaeleweka

Ufanye mwongozo uwe mfupi kwa kadri iwezekanavyo na uandike maana au mawazo muhimu tu. Tumia buleti na jadulweli vya maandishi ili kuokoa nafasi, lakini onyesha mawazo muhimu.

### Tumia mifano kutoka kwenye Mwongozo wa Mwalimu

Waache walimu watumie mwongozo halisi wa mwalimu wa programu na maandalio ya somo katika mafunzo haya. Chukua muda kuwaonyesha walimu mwongozo wa mwalimu; eleza kuhusu alama zilizotumika na muundo ya mwongozo kwa ujumla. Kisha, kwa kila kitendokitakachotekelezwa, waelekeze walimu waifanyie mazoezi tumia mifano mahususi kutoka kwenye mwongozo. Walimu wataujua mwongozo wa mwalimu au hati zingine wakati wakijifunza mazoezi mengine ya ufundishaji.

### Tenga muda wa kutosha kwa kila kitendo

Hakikisha wakufunzi wanajua muda kamili ambao kila kitendo kitatumia. Ajenda ya mwanzoni mwa mwongozo wa mafunzo husaidia; kitakachosaidia zaidi ni kuhakikisha unatumia muda uliopangwa kwa kila kipindi au kitendo kuelekea katika mwongozo wa mafunzo.

### Panga muda wa ziada

Zingatia kuwa hata mafunzo yaliyopangwa vema pamoja na kutumia wakufunzi wenye uzoefu Zaidi, mafunzo yanaweza Kwenda nje ya ratiba. Maswali watakayouliza walimu, kutembelea maofisa wa serikali vinaweza kuchukua muda zaidi kuliko ilivyotarajiwa. Pia, baadhi ya teknolojia zinaweza kufeli na kusababisha Kwenda nje ya muda Kutenga muda wa ziada kwa kuongeza muda zaidi ya ule unaohitajika au kwa kuepuka vitendo kama za kujichangamsha kama itahitajika. Onyesha vitendo ambavyo si vya lazima ambayo wanaweza kuviepuka

### Wahusishe washirika kutoka wizarani kwa wingi kadri iwezekanavyo

Utengenezaji wa mwongozo wa mafunzo ni fursa nzuri ya kuwahusisha washirika kutoka Wizarani Kuihusisha Wizara katika hatua hii kutasaidia katika kuto usimamizi wa serikali, utajenga uelewa wa mbinu za ufundishaji, na utahakikisha uendelevu wa mradi. Ushiriki wa washirika kutoka Wizarani, kunaweza pia kuboresha kusimamia mafunzo hayo na pia kusaidia kuonesha umuhimu wa mafunzo ambayo ambayo bila shaka kutazidisha kujenga hamasa zaidi miongoni mwa walimu.

MIONGOZO ILIYO BORA YA MAFUNZO INASAIDIA KUDHIBITI UJUMBE KUTOBADILIKA

## MBINU ZA MAFUNZO

**Mbinu za mafunzo ndio vitendo vinavyotumika katika ufundishaji zinazotumika kuwasilisha maudhui katika mafunzo. Kwa kawaida kuna njia kuu nne zinazotumika katika mafunzo – mihadhara, mijadala, kuigiza na kufanya mazoezi, ambazo zitaelezwa katika sehemu hii. Mbinu zinazotumika katika kuwasilisha maudhui ni muhimu kama yalivyo maudhui yenyewe. Ujifunzaji wa watu wazima unapaswa kujumuisha mbinu za kujifunza kwa vitendo; watu wazima wanajifunza vema kwa kutenda. Zingatia jinsi ya kuwafanya walimu "kutenda" kama njia ya ufundishaji wakiwa kwenye mafunzo ili waweze kujaribu mbinu mpya darasani kwa kujiamini zaidi.**

### Mazoezi

Hii ni mbinu muhimu zaidi ya kufundishia umbinu mpya za ufundishaji kwa sababu kuu mbili. Kwanza, kuwa na wazo thabiti la shughuli ambazo zinaonekana kama walizijaribu huko nyuma darasani, kutawafanya walimu kujiamini katika kulifanya hili kwa mafanikio. Pili, walimu wanapaswa kushughulikia masuala mbalimbali huku pia wakifundisha, na kadiri wanavyozifanyia kazi kwa ukaribu zaidi hatua wanazopitia katika kufundisha, ndivyo watakavyoweza kushughulikia mahitaji ya kujifunza ya wanafunzi wao wakati wa kufundisha.[4] **Muda zaidi wa mafunzo unapaswa kutumika kwenye mazoezi kuliko kitu kingine chochote. Mazoezi hayayanapaswa kufanyika katika wakiwa katika jozi au vikundi vidogo kuliko katika vikundi vikubwakundi kubwa.** Umuhimu wa kikundi kidogo au mazoezi ya jozi hauwezi kupuuzwa: Kila mwalimu anapaswa atenge nafasi ya kufanya mazoezi kila kitendo. Utafiti wa RTI uligundua kwamba kwa uwastani, ni asilimia 60

JINSI MAUDHUI YANAVYOWASILISHWA NI MUHIMU KAMA VILE YALIVYO MAUDHUI YENYEWE

tu ya walimu waliweza kufanyia mazoezi mafunzo waliyopewa kwa sababu mengi ya mazoezi hayo yalifanyika katika vikundi vikubwa na hivyo ikaruhusu mwalimu mmoja au wawili kufanyia mazoezi katika muda uliopangwa. Hivyo, kuhakikisha kuwa kila mwalimu anapata muda wa kufanyia mazoezi kila kitendo na kufanya mazoezi katika jozi kuliko vikundi kutahakikisha kila mwalimu anakuwa na muda wa kutosha wa kufanya mazoezi

## Mitindo

Uelewa wa kina juu ya maarifa mapya ni kule kuona kipi kinapaswa kuwa namna kinavyopasa kuwa Kutoa mifano ya mazoezi ya ubora wa hali ya juu kwa kila kitendo kutasaidia kuwapa walimu wazo la kile wanacholenga kufanya katika ufundishaji wao. Kwa kutumia igizo la ufundishaji lenye ubora ubora hali ya juu, kunaweza kuwa bora zaidi kkwa kufanywa na mwalimu mzuri sana wa kawaida kuliko kufanywa na mkufunzi.

## Mjadala

Matumizi bora ya njnia ya mjadala hufanywa kwa kujibu maswali ambayo walimu wanayo na kuruhusu walimu kujadili uzoefu wao darasani na wakati wa mafunzo, ili kusaidiana kutatua changamoto zinazowakabili. Mijadala pia inaweza kutumika kama nafasi ya kujitafakari au kujitathmini. Ni rahisi kwa mijadala kutumia muda zaidi ya uliopangwa, kwa hiyo kuweka uwiano mzuri wa mijadala na muda ni muhimu.


## Mihadhara

Mihadhara inaweza kuwa muhimu katika kufafanua dhana na maana za istilahi. Hata hivyo, ni njia yenye ufanisi mdogokabisakatika kuwasaidia walimu wajiandae kufundisha dhana/ kitu kipya Panga muda mchache sana katika kutumia mbinu ya mijadala

Kwa kuzingatia mbinu hizi kuu nne za za ufundishaji unawezaje kuamua ni kwa kiasi gani unaweza kuitumia kila moja wapo? Utafiti wa ndani wa RTI uligundua kwamba walimu wanapendelea mbinu ya mazoezi na mitindo. Miradi inayoleta matokeo mazuri ya wanafunzi inaonesha kuwa wanafunzi walianza kutumia mazoezi zaidi katika mafunzo yao.

Kielelezo cha 1 kinaonyesha njia moja ya kuzingatia juu ya namna kutumia muda kati ya njia hizi kuu nne, lakini kuamua juu ya njia bora bora kutategemea sana maudhui ya somo.

**KIELELEZO CHA 1.**
**Mapangilio wa muda wa mafunzo unaopendekezwa**




> "NAJISIKIA KUJIAMINI. KUFANYA KWA MAIGIZO NA KUFANYA KWA VITENDO NA KUTOKUONA AIBU KUMENIFANYA NIWEZE KUFUNDISHA KAMA MWALIMU MWINGINE YEYOTE. IMENIFANYA NIJISIKIE KUJIAMINI."
> MWALIMU WA TUSOME

## TARATIBU ZA MAFUNZO NA MAHITAJI YAKE

**Matayarisho kwa ajili ya mafunzo ya walimu, hususan ya yanayowahusisha watu wengi na ya viwango tofauti , lazima YAANZE MAPEMA. Kuna maamuzi muhimu mbalimbali na kufanya mambo mbali mbali bila uhakika. Kwa hivyo kadiri utakavyokuwa na muda mwingi wa kufanya maandalizi, ndivyo utaweza kurekebisha kasoro ndogo ndogo hadi utakapofanikisha lengo lako. Programu zenye ufanisi hutekelezwa ndani ya mifumo ya serikali ili kuoanisha muda unaotumika kwa mafunzo na kalenda kuu ya jumla ya mafunzo ya walimu ili kupunguza kurudia rudia. Maamuzi muhimu ni pamoja na:**

### Mafunzo kwa nia ya kuambukizana au laa

Huu ni uamuzi wa kwanza muhimu wa kufanya. Katika mtindo wa mafunzo ya kuambukizaqna, timu ya wakufunzi mabingwa, huwafundisha wakufunzi wa walimu ili nao wakawafundishe walimu huko chini. Mtindo wa mafunzo ya aina hii hutofautiana kutegemea idadi ya walimu wanaaohisika na muda uliopo. Mtindo usio kuwa wa maambukizi unamaanisha kwamba, kikundi kiomja cha wakufunzi watafundisha walimu moja kwa moja, jambo ambalo linaweza kuchukua muda mrefu zaidi kutegemea na idadi ya walimu watakao fundishwa na kiwango cha ujuzi cha wakufunzi wenyewe. Kutumia njia ya maambukizi kufundisha walimu wengi zaidi na kwa haraka, lakini kadiri unapokuwa na ngazi ntingi za wakufunzi ndivyo ujumbe wa mafunzo unavyoweza kuzimuliwa Kwa mazingira Fulani mtindo wa maabukiziunaweza kuwa ndio njia pekee ya kutumia. Inashauriwa kupunguza yawing wa hatua na pia hakikisha kwamba hatua zote zinapata mafunzo ya aina moja. Njia rahisi zaidi ya kupunguza idadi ya hatua ni kuyafanya mafunzo kwa kipindi kirefu Zaidi ili kwamba wakufunzi mabingwa na wakufunzi wa walimu waweze kutoa maudhui kamili nay a aina moja kwa walimu kutoka maeneo mengi zaidi Fanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa mafunzo kwa

**TEKNOLOJIA NA MBINU ZA MAFUNZO**

Kuna njia nyingi za kuzingatia ikiwa ni pamoja na kuiona teknolojia kama sehemu ya mafunzo yenyewe kama vile kutumia PowerPoint au video katika kuwasilisha dhana, kusaidia katika kutafanya mafunzo yaweze kutekelezeka. **Hata hivyo, kabla ya kubuni shughuli zinazotegemea teknolojia, zingatia kwa makini maudhui na kiwango cha ufahamu wa teknolojia kwa washiriki.** Je, eneo litakuwa na umeme? Wifi? Je, nafasi ni kubwa kiasi gani? Je, washiriki WOTE wamezoea kutumia simujanja? Vishkwambi? Kutegemea majibu ya maswali haya, kunaweza kusiwe na teknolojia inayoweza kufaa. Maamuzi yoyote yatakayofanywa yanapaswa kuzingatia kwamba teknolojia inapaswa kuwa zana ya ujifunzaji, mada kuu ya ujifunzaji.

wakufunzi hayafupishwi Pia panga kuwa na walimu wasiozidi 30 kwa kila wakufunzi 2, kama inawezekana. Kuwa na walimu wachache zaidi ni bora, lakini hii hutegemea idadi ya walimu na uwiano wa maafisa wanaoshughukia ufundishaji.

## Nani wanahusika kwenye mafunzo

**Mwalimu yeyote anayekwenda anaefundisha anapaswa kuhudhuria mafunzo haya**. Wakati mwingine skuli au programu huamua kufundisha mwalimu mmoja kwa kila skuli, wakitarajia mwalimu huyo atawafundisha pia walimu wengine. Kuna masuala mawili hapa. Kwanza, mwalimu huyo hatakuwa mtaalamu wa maudhui au njia za mafunzo baada ya kupata mafunzo ya mara moja. Pili, hakuna njia ya kuhakikisha kwamba mwalimu huyo anawafundisha walimu wengine vizuri – au kaa atawafundisha kabisa. Walimu wakuu au wakurugenzi waskuli wanapaswa kuhudhuria angalau sehemu ya mafunzo haya. Kadri wakavyofahamu kuhusu mbinu za ufundishaji, ndivyo watavyoweza kuunga mkono zaidi jambo hili. Faiida ya ziada kwa kuwa na walimu zaidi ya mmoja ni kwamba walimu wataweza kusaidiana baada ya mafunzo wakati wakijifunza kutumia njia mpya darasani.

## Mpango wa uhamasishaji kwa wakufunzi

Unapopanga mafunzo, hususan kwa mafunzo yanayowahusisha walumu wengi ni muhimu kuwa na mpango ulioandaliwa tayari kwa kila mkufunzi, ikiwa ni pamoja na mahali, tarehe, na kiwango cha mafunzo. Utekelezaji wa mafunzo ya makubwa unaweza kuhusisha mamia ya watu wanaosafiri kwenda kwenye maeneo ya mafunzo nchi nzima. Kuhakikisha nani anakwenda wapi na katika siku gani kunahitaji mfumo nzuri, kama vile majedwali ya Excel.

## Udhibiti wa ubora

Hakikisha ujumbe haubadiliki katika hatua zote za mafunzo. **Kila mafunzo yanapaswa kuwa na mtu wa kusaidia katika kudhibiti wa ubora** . Huyu anapaswa kuwa mtu mwenye uzoefu wa mafunzo. Anaweza kuwa mfanyakazi wa programu au wizara mwenye uzoefu ambaye anaweza kusaidia wafanyakazi wengine wakati wakiwafundisha walimu. Mtu huyu anatakiwa aweze kubaini suala lolote linalohusiana na ubora wa mafunzo na hata kuingia kusaidia kufundisha inapohitajika. Kuza orodha rahisi ya nyenzo ambayo mtu wa udhibiti wa ubora anaweza kutumia ili kukusanya data juu ya namna mafunzo yanafanyika. Hii itasaidia kukabiliana na changamoto zozote kwa kuzitatua kwa haraka.

## Mafunzo ya kulalaau yasiyo ya kulala

ni jambo ambalo linapaswa kufikiriwa kwa kina Utafiti uliofanywa kupitia Mradi wa Kisomo na uendelevu wa wanafunzi katika skuli zao nchini Uganga (Literacy Achievement and Retention Activity in Uganda) uliangalia juu ya faida na hasara za mifumo yote miwili .[5] Utafiti huo ulilinganisha gharama pamoja na masaa ya mafunzo nakiwango cha ujifunzaji. Uligundua kwamba mafunzo yaliyotumia njia ya kulala katika maeneo ya mafunzo yalikuwa na gharama zaidi na kimsingi hayakuwaongezea maarifa ya walimu. Gharama za ziada za mafunzo ya ya kulala hazikutoa thamani stahiki kwa athari yake ndogo yakliyotoa.

## Mafunzo ya wakufunzi

Wakufunzi ndio wanaoathiri sana mafanikio ya mafunzo. Wanapaswa wayaishi mafunzo kama vile ambavyo wao watayatoa. Hili wanalijua. Maudhui ya nyongeza yaliyojikita katika jinsi ya kutoa mrejesho kwa ufanisi juu ya ujifunzaji wa watu wazima na uwezeshaji mbinu za uwezeshaji yatakuwa muhimu. Uwezekano ni kwamba wakufunzi hawatakuwa walimu wa skuli ya msingi wenye uzoefu au wenye utaalamu wa kisomo/hesabu za msingi. kwa hiyo mafunzo wanayopokea yatakuwa muhimu kwa mafanikio ya mafunzo ya walimu. Kwa mafunzo ya kina, kwa kiasi inavyowezekana, panga wakufunzi wawili kwa kila mafunzo. Tumia wakufunzi wa wizara au wafanyakazi wengine wanaofaa kuwa wakufunzi. Wanaweza wasiwe wataalamu wa maudhui hayo, lakini kwa mafunzo ya vitendo na udhibiti ubora, watafaa. Washauri wa walimu wanaweza kuwa wakufunzi pia. Tazama Mwongozo wa 6 mafunzo endelevu kwa kuhusu ufundishaji wa walimu. Hii itawasaidia kukuza uhusiano na walimu na kuelewa kwa kina kuhusu ufundishaji. Au, fikiria kutumia walimu weledi Zaidi na wakufunzi kama mifano. Walimu wataonesha mifano bora kwa kuwa wao ndio wanaoyaelewa vema madarasa.

FIKIRIA KUWATUMIA WALIMU WENYE UZOEFU NA WAKUFUNZI KAMA MIFANO

Wakati mwongozo huu umejikita katika kuandaa na kutoa mafunzo ya kazini yenye ubora katika programu za ufundishaji, ni muhimu kuhakikisha kwamba mafunzo yanakuwa endelevu wakati wote. Kushirikiana na maofisa na wafanyakazi wa wizara wakati wote, kama ilivyojadiliwa hapo juu , kutasaidia sana. Kwa kuongezea, juhudi zinapaswa kufanywa ili kuhakikisha kwamba programu ya mafunzo haya inaingizwa kwenye mfumo wa serikali, ikiwa ni pamoja na kutambua walimu wanaofanya vizuri na kutafuta fursa za kuyaunganisha mafunzo haya katika program za vyuo vya mafunzo ya ualimu

## NOTISI ZA MWONGOZO

Mwaka 2017–2018 RTI ilifanya utafiti wa kitaifa kuhusu programu za RTI za mafunzo ya walimu na kupata muhtasari wa majibu hayo kwa mwongozo ufuatao:

Mwongozo Muhimu wa Mafunzo:

1. Punguza wingi wa maudhui kwenye mafunzo.
2. Ongeza muda uliotengwa kuigiza na kufanya mazoezi.
3. Uigizaji wa ujuzi unapaswa kufanywa na wawezeshaji mahiri.
4. Tengeneza muundo wa mwongozo wa mafunzo ili kuongeza urahisi wa kutumia.
5. Fundisha mbinu za utunzaji wa muda kwa wawezeshaji na wafanyakazi wengine wa programu.
6. Hakikisha wawezeshaji wanaelewa nadharia ya maadiliko inayohusiana na program hii.
7. Miongozo ya mafunzo, miongozo ya walimu na vitabu vya kiada vya wanafunzi vinapaswa kuwa nyenzo muhimu zitakazotumika.

Mwongozo wa Mafunzo Uliopendekezwa:

8. Miongozo ya mafunzo inapaswa kutoa mwongozo ulio mahsusi, rahisi na ulio wazi.
9. Jumuisha muda wa nyongeza wakati wa kupanga muda katika mwongozo wa mafunzo.
10. Fuata mwongozo wa mafunzo kwa wakufunzi mahiri na Mafunzo ya Wakufunzi.
11. Weka vigezo katika kuchagua wawezeshaji.
12. Sisitiza vipengele 5 kusoma na kuandika.

## HITIMISHO

Uzoefu husaidia katika kupanga mafunzo ili yafanikiwe kadri iwezekanavyo. Kuzingatia mazingira na kanuni za ujifunzaji wa watu wazima wakati wote wa mchakato kutasaidia kuhakikisha walimu wako tayari kutumia nyenzo mpya katika madarasa yao baada ya mafunzo kuisha. Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka, kwamba jambo hili hutumia muda: walimu hawataweza kuyatekeleza kwa ukamilifu katika wiki ya kwanza au hata muhula. Kujifunza na kukamilisha ufundishaji kunahitaji mrejesho wa mara kwa mara. Uzoefu ulioandikwa kwa muhtasari katika notisi za mwongozo hapo juu, yataendelea kuwasaidia walimu kwa muda mrefu sana kadri iwezekanavyo.

Kuhusu alama zilizotumika katika mwongozo huu:

Huonyesha "Tahadhari ya Hatari": Kitu cha kukijua na tahadhari nacho, kwa sababu ni tatizo la kawaida

Huonyesah "Isiyo na mjadala": lazima kuwa nayo

## RASILIMALI

**Uwasilishaji wa CIES 2019 Ufundishaji wa walimu au roboti: Matokeo yasiyotarajiwa ya utafiti kutoka nchi 7 kuhusu mendeleo ya taaluma ya mwalimu:**
https://shared.rti.org/content/training-teachers-or-robots-unexpected-findings-7-country-teacher-professional-development

**Darling-Hammond and Richardson on "Research Review/Teacher Learning: What Matters?":**
http://www.ascd.org/publications/educational-leadership/feb09/vol66/num05/Teacher-Learning@-What-Matters%C2%A2.aspx

**Knowles on *Andragogy in Action: Applying Modern Principles of Adult Learning*.**

**Uwasilishaji wa CIES 2019 mafunzo Madogo yasiyo kuwa ya kulala dhidi ya mafunzo makubwa ya makazi:**
https://shared.rti.org/author/tiguryera-s

**Semina ya mtandaoni juu ya mafunzo ya kazini na msaada wa walimu unaoendelea:**
https://www.globalreadingnetwork.net/events/continuous-professional-development-early-grade-reading-programs

**Complete Series of Structured Pedagogy How-To Guides:** https://scienceofteaching.site/how-to-guides/

MAREJELEO

1 Malcolm S. Knowles, Andragogy in Action: Applying Modern Principles of Adult Learning (San Francisco: Jossey-Bass, 1984)
2 David F. Feldon, "Cognitive Load and Classroom Teaching: The Double-Edged Sword of Automaticity," *Educational Psychologist* 42, no. 3 (December 5, 2007): 123–137, DOI: 10.1080/00461520701416173
3 Benjamin Piper, Jessica Mejia, Jennifer Spratt, Yasmin Sitabkhan, Kellie Betts, Patience Sowa, and Wendi Ralaingita, *Teacher Professional Development in Low- and Middle-Income Countries: Results of the 17-Country Teacher Study Examining Survey Findings, Training Manual Analysis, and Observations of Teacher Training* (Research Triangle Park, NC: RTI Press, forthcoming).
4 Feldon, "Cognitive Load," 2007.
5 Small non-residential trainings vs. large residential training: Findings from action research in Uganda [CIES 2019 Presentation] https://shared.rti.org/content/small-non-residential-trainings-vs-large-residential-training-findings-action-research

Hati hii imepewa leseni chini ya Leseni ya Kimataifa ya Hatimiliki Inayoruhusu Umma Kunakili, Kusambaza, na Kuboresha Maudhui Jinsi Wapendavyo 4.0.
https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

Mwongozo umeandikwa na **Jessica Mejía**